

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

**CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU**

**NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA YA VIWANDA VYA MISITU KWA**

**MWAKA WA MASOMO 2022/2023**

Mkuu wa Chuo cha Viwanda Vya Misitu Misitu kilichopo Moshi, Mkoani Kilimanjaro. Anatangaza nafasi ya mafunzo ya teknolojia ya viwanda vya misitu katika ngazi za Astashahada (Cheti) na Stashahada (Diploma) kwa mwaka wa masomo 2022/2023.

**A. Kozi zinazotangazwa:**

- i. Astashahada ya Awali ya teknolojia ya viwanda vya misitu (NTA – Level 4) mafunzo ya mwaka mmoja (1);

**Sifa za mwombaji:**

- Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya sekondari na ufaulu wa alama D katika masomo manne;
- Masomo mawili kati ya hayo aliyofaulu yawe aidha Baiolojia au Kemia au Fizikia au Hesabu au Jiografia;
- Ufaulu wa somo la kiingereza utakuwa kipaumbele cha ziada katika uchaguzi.

- ii. Astashahada ya teknolojia ya viwanda vya misitu (NTA – Level) mafunzo ya mwaka mmoja; (1);

**Sifa za mwombaji:**

- Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu Astashahada ya awali ya teknolojia ya viwanda vya misitu au Astashahada ya awali ya ufugaji nyuki au fani nyingine inayolandana na hizo kutoka chuo chochote kinachotambulika na Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET); AU
- Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya juu ya sekondari na awe na amesoma michepuo ya sayansi na kufaulu katika masomo mawili kwa alama ya E na S;

- iii. Stashahada ya teknolojia ya viwanda vya misitu (NTA – Level) mafunzo ya mwaka mmoja (1);

**Sifa za mwombaji;**

- Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu Astashahada ya teknolojia ya viwanda vya misitu au fani nyingine ya sayansi inayolandana na hizo kutoka chuo chochote kinachotambulika na Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET);

## **B. Jinsi ya Kutuma maombi:**

- I. Mwombaji atatakiwa kujaza fomu, kusaini na kuituma fomu ya maombi ikiwa na vielelezo vyote muhimu kama cheti cha kumaliza elimu ya sekondari, cheti cha kuzaliwa na fomu ya daktari;.
- II. Fomu za maombi zinapatikana Chuo cha Viwanda vya Misisu, Moshi au kwenye tovuti ya chuo (<http://www.fiti.ac.tz>);
- III. Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi na taarifa za matokeo katika lugha ya Kiingereza. Endapo mwombaji atakuwa na Ufadhiri, uthibitisho wa maandishi kuhusu Ufadhiri huo utahitajika;
- IV. Ada ya maombi ya kujiunga na chuo ni Shilingi za Kitanzania 10,000/= (elfu kumi) kwa Watanzania ma Dola za Kimarekani 20.00 kwa wasio Watanzania;
- V. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi kupitia **control number**.

## **C. Kuomba *control number* andika mahitaji yafuatayo;**

- Jina kamili la mwombaji kama linavyosomeka kwenye cheti cha O-level au results slips;
- Andika namba ya simu ya mwombaji/mzazi/mlezi;
- Anwani ya mwombaji;

Tuma taarifa hizo kwa njia ya **SMS** kwa namba zifuatazo au kupata ufafanuzi zaidi, mwombaji/mzazi/mlezi awasiliane kwa namba zifuatazo;

- (i) Afisa udahili wa chuo – **0755771852**
- (ii) Mhasibu wa Chuo - **0717085141**
- (iii) Mratibu Mkuu wa Mafunzo - **0752206305**

## **D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI;**

- I. Fomu ya mombi inapatikana kwenye tovuti ya chuo ([www.fiti.ac.tz](http://www.fiti.ac.tz)) na Maombi yote yatumwe kupitia anwani ifuatayo:- [admission@fiti.ac.tz](mailto:admission@fiti.ac.tz) au **S.L.P 1925 MOSHI**

## **E. TAHADHARI**

- I. Kwa yeyote ambaye hatazingatia utaratibu uliotajwa hapo juu, maombi yake hayatafikiliwa. Aidha , mwombaji atakayewasilisha hati za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria ;
- II. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **15 Agosti 2022**.

## **F. TAARIFA KWA WATAKAOCHAGULIWA;**

- ❖ Majina ya wataochaguliwa pamoja na maelezo ya kujiunga na chuo yatawekwa kwemye tovuti ya Chuo (<http://www.fiti.ac.tz>);

**“WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA MNAKARIBISHWA”**